

**OFISI YA RAIS
TAMISEMI – DODOMA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KONGWA**

SHULE YA SEKONDARI NDALIBO,
S. L. P 132,
KIBAIGWA,
09/12/2020.

Simu : 0627-202-428 - Mkuu wa shule
Mail : ndalibosecondaryict@gmail.com

KUMB. NA. NDB/SS/JI.2021.NO 12
JINA LA MWANAFUNZI :.....
S. L. P.....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NDALIBO WILAYA YA
KONGWA MKOA WA DODOMA JANUARI 2021.**

1.0 UTANGULIZI

Ninafuraha kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021, shule ya sekondari Ndalibo ipo umbali wa kilometra kumi na tano (15km) kutoka barabara ya rami, kata ya mtanana.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021 mwisho wa kuripoti ni tarehe 18/01/2021 (ndani ya siku saba).

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 SARE ZA SHULE

Wavulana

- a) Suruali damu ya mzee na shati jeupe la mikono mifupi.
- b) Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi
- c) Soksi nyeusi.

Wasichana

- a) Sketi damu ya mzee linda box na sio V na shati jeupe la mikono mifupi.
- b) Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi
- c) Soksi nyeupe.

2.2 VIFAA VYA KUSOMEA NA USAFI

- a) Madaftari kumi na nane (18)
- b) Kalamu nyeusi au bluu
- c) Kamusi ya kингереza – Kiswahili
- d) File moja (1) la kaki
- e) Mkebe wa hisabati na rula
- f) Msichana aje na fyekeo jipya, ufagio wa chelewa mpya na ndoo mpya

g) Mvulana aje na jembe jipya, ufagio wa chelewa mpya na ndoo mpya

2.3 MAHITAJI MENGINE

- a) Aje na kiti na meza au pesa Tsh. 60,000/= kwa ajili ya matengenezo ya kiti na meza.
- b) Bunda la karatasi 1 (Rim paper 1) kwa ajili ya majoribio ya kila wiki na kila mwezi.

2.4 MICHANGO YA CHAKULA

Kila mwanafunzi aje na mahindi debe 1 na nusu, maharage kilo 6 na fedha Tsh. 15,000/= (Elf u kumi na tano tu) kwa ajili ya kununua mafuta ya kupikia, nyanya, vitunguu, sufuria na kumlipa mpishi (chakula cha muhula mmoja) miezi sita (6), Lishe kwa mwanaao shuleni ni muhimu sana kwa maendeleo ya taaluma.

3.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule inaongozwa kwa mujibu wa sharia Na. 25 ya mwaka 1978. Mwanafunzi atapaswa kusoma, kuzielewa na kuzifuata sharia na kanuni za shule. Makosa yafuatayo yatakayosababisha mwanafunzi kusimamiswa masomo au kufukuzwa shule:

- a) Kubeba ujauzito au kusababisha ujauzito
- b) Kutoa mimba au kusaidia kutoa mimba
- c) Wizi
- d) Uasherati na ubakaji
- e) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyta
- f) Uvutaji wa bangi na sigara
- g) Kupigana au kupiga
- h) Kugoma au kuchochea na kuongoza kuvuruga amani na usalama wa shule
- i) Maneno machafu (matusi)
- j) Kutoka nje ya shule bila ruhusa ya mwalimu
- k) Kuhalibu kwa makusudi mali ya umma (shule)
- l) Kutofanya mitihani au wizi wa mitihani
- m) Utoro wa reja reja.

“ELIMU KWA MAENDELEO”

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI NDALIBO

Ahsante

.....
MUHURI